

N E W

08/03/2022

HALMASHAURI YA WILAYA YA MUHEZA
(Barua zote ziadikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)
S.L.P 20,
MUHEZA.

Namba ya Simu: 027 2641105,
Namba ya Fax: 027 2641414
Barua pepe: ded@muhezadc.go.tz
Tovuti: www.muhezadc.go.tz

Kumb.Na.HW/MUH/L.90/21/VOL. II/55

07/03/2022

**TANGAZO LA AJIRA ZA MUDA ZA KUKUSANYA TAARIFA NA KUWEKA ANWANI
ZA MAKAZI WILAYA YA MUHEZA**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza anapenda kuwatangazia wananchi wote nafasi za ajira za **MUDA** za kazi ya kukusanya Taarifa na kuweka Anwani za makazi katika kata zote na vijiji vyote katika Halmashauri ya Wilaya ya Muheza.

A: SIFA ZA MWOMBAlJ

- i. Awe raia wa Tanzania mwenye umri kati ya miaka 18 – 35
- ii. Awe na elimu ya kidato cha NNE na kuendelea
- iii. Awe anamiliki simu Janja (**Smartphone**) yenyе Teknolojia ya **Android** kuanzia **version 6.0** na kuendelea na yenyе uwezo wa kukaa na chaji muda mrefu, na yenyе uwezo wa kuchukua majira ya nukta (coordinates) chini ya **digrii 4.00**
- iv. Awe na barua pepe (email address) na (nywila) Password inayofanya kazi.
- v. Awe na uwezo wa kusoma ramani za mitaa, majengo, barabara na kutafsiri. Wenye Taaluma ya TEHAMA au usomaji wa ramani watapewa kipaumbele.
- vi. Awe mkazi wa kata na kijiji husika.
- vii. Awe mwaminifu na mwadilifu na mchapakazi na aweze kufanya kazi kwa kuzingatia muda uliowekwa.

N E W

V

B: KAZI NA MAJUKUMU

- i. Kukusanya taarifa za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma
- ii. Kukusanya taarifa za wamiliki wa nyumba, wategemezi, viwanja na maeneo ya huduma kwa kutumia Mfumo wa anwani za makazi.
- iii. Kutuma taarifa kwenye mfumo wa anwani za makazi
- iv. Kuandika namba za anwani kwenye nyumba au majengo.
- v. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na msimamizi wa kazi.

C: MAOMBI YAAMBATANISHWE NA:

Mwombaji anatakiwa kuambatanisha maombi yake na vitu vifuatavyo;

- i. Nakala ya cheti cha kidato cha NNE na kuendelea
- ii. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
- iii. Picha (Passport size 2)
- iv. Vyeti vya Taaluma
- v. Nakala ya kitambulisho cha Taifa (NIDA)

D: JINSI YA KUTUMA MAOMBI

Barua zote za maombi ziandikwe kwa usahihi zikioneshwa anwani kamili ya mwombaji, namba ya simu, barua pepe na kijiji anachotoka. Pia barua zipitie kwa **Mtendaji wa Kijiji na Kata** husika kwenda kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Muheza. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe ni Tarehe **14/03/2022 saa 9:30** alasiri

Nassib B. Mmbagga
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
MUHEZA

MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA MUHEZA

08/03/2022